



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI
TANZANIA



TAARIFA KWA UMMMA

**KUREJEA KWA SHUGHULI ZA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA
AFRIKA MASHARIKI (EACOP)**

26.06.2020

Hivi karibuni Kampuni ya kimataifa ya mafuta ya TOTAL, ilitangaza kufikia makubaliano katika ununuzi wa hisa zote za Kampuni ya Tullow ambayo ilikuwa mmoja ya wabia katika mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (East Africa Crude Oil Pipeline-EACOP).

Kufuatia makubaliano haya, zabuni zote za mradi ambazo zilikuwa zimesimamishwa zinatarajiwa kurejea kutangazwa tena (*Call for tender re-launch*) hivi karibuni na kufikia mwezi wa Septemba, 2020 mazungumzo yote kati ya wabia wa mradi na Serikali ya Uganda na Tanzania yanatarajia kuwa yamekamili. Maamuzi ya mwisho ya uwekezaji katika mradi (FID) yanatarajiwa kutolewa na wabia ifikiapo mwezi Desemba, 2020 ambapo ujenzi wa miundombinu ya mradi unatarajiwa kuanza mapema mwanzoni mwa mwaka ujao wa 2021.

Kampuni ya TOTAL kwa niaba ya Kampuni ya ubia (EACOP co) ndio ina wajibu wa usimamizi wa kazi mbalimbali za mradi wa EACOP. Kampuni hiyo pamoja na majukumu mengine ndiyo yenye jukumu la kutoa taarifa za mradi ikiwemo zabuni pamoja na ajira kulingana na makubaliano yalioingwa na wabia wa Mradi wa EACOP.

Hata hivyo, tayari kumeanza kuibuka makampuni binafsi pamoja na watu wasio waaminifu kwa kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusiana na utangazaji wa zabuni pamoja na ajira zinazotarajiwa kupatikana katika mradi.

TPDC kama mshirika mkuu na mbia katika mradi kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, inapenda kuutaarifu umma ya kwamba, zabuni zote za mradi zitatangazwa na kampuni ya TOTAL ambayo ndiyo kampuni mbia iliyopewa dhamana ya kufanya hivyo na kwamba hakuna mtu wa kati ama dalali ambaye amepewa jukumu hilo. Hata Hivyo TPDC inashauri watoa huduma katika miradi ya mafuta na gesi wajiandikishe katika kanzi data ya EWURA kwani ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia ushiriki wa Watanzania katika miradi mikubwa ya gesi na mafuta ili watambulike.

Taarifa zote za mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki zinapatikana katika tovuti ya kampuni ya EACOP ambayo ni **www.eacop.com** au tovuti ya TPDC **www.tpdc.co.tz** ambapo *link* yenye kuonesha shughuli zote za mradi inapatikana.

Hivyo TPDC inapenda kuusisitiza umma kuendelea kufuatilia habari za mradi katika vyanzo sahihi vilivyoelezwa na kuepuka matangazo ambayo tayari yameanza kutolewa na watu binafsi pamoja na makampuni ambayo hayahusiki katika mradi huu.

Imetolewa na

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano,

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

"Ujenzi wa Bomba la mafuta: Tumeamua na Tunatekeleza"